# MWONGOZO
# WA
# KUHARIRI WIKIPEDIA

*WIKIMEDIA FOUNDATION*
*NA*
*JENGA WIKIPEDIA YA KISWAHILI AFFILIATE*

# Utangulizi

**Wikipedia** ni kamusi elezo katika intaneti inayojengwa na jumuiya ya washiriki nawe unaweza kuchangia. Mwongozo huu utakusaidia kuwa mchangiaji wa Wikipedia.

Kurasa zifuatazo zitakupa mwongozo kuhusu mtindo na makala za Wikipedia zilivyo, na kukuelezea kuhusu jumuia ya Wikipedia na sera muhimu za Wikipedia na makubaliano.

Huu ni mwongozo wa kimsingi tu, na siyo maelekezo ya kirefu. Iwapo unataka maelezo zaidi, kuna viungo kuelekea kurasa nyingine kwa maelezo zaidi. Kuzisoma na kuzielewa, unaweza ukazifungua katika kivinjari tofauti au katika dirisha la tabo.

Kuna viungo kuelekea katika kurasa za "sanduku la mchanga" ambapo unaweza kujipatia uzoefu kile unachojifunza. Hebu jaribu vitu tofauti na uchezecheze! Hakuna mtu atakayechukizwa endapo utavuruga na jaribio katika maeneo ya vitendo.[1]

---

[1] **Ilani**: Mwongozo umetoa maelezo yanayofaa hasa kwa wale wanaotumia umbo la kurasa la MonoBook. Tangu Septemba 2010 umbo la kurasa kama inavyoonekana kwa watumizi wasioingia akaunti ni Vector. Mwongozo bado haujaandikwa upya. Wale walioingia akaunti zao wanaweza kubadilisha umbo la kurasa kwenye mapendekezo yao. Umbo nyingine zinaweka viungo mahali

# Kuhariri

Ukurasa huu unaeleza hali ya kihariri cha kawaida (wiki-text-editor). Kwa kutumia **kihariri oneshi** (VisualEditor) bofya **hapa** (ukiona maandishi mekundu, maana yake ni kwamba haijaandaliwa).

Unaweza kuhariri kila ukurasa wa Wikipedia yaani kusahihisha, kuongeza habari, kuziondoa au kuzibadilisha. Karibu kila ukurasa una kiungo kinachosema "***hariri chanzo***", ambacho kinakupatia nafasi ya kubadilisha ukurasa unaotazama. *(Kurasa chache zinalindwa hazikupi nafasi hii.)*

Hiki ni kipengele muhimu sana cha Wikipedia, na wote wanaruhusiwa kuhariri. Iwapo unaongeza habari fulani kwenye makala, tafadhali weka marejeo, kwa sababu habari zisizo na uthibitisho kuna uwezekano mkubwa wa kuondolewa. Pia ni ushauri mwema kwamba kutafuta majadiliano kwenye ukurasa wa majadiliano kama unataka kuleta mabadiliko makubwa hasa ukiona mwandishi aliyetangulia alikosea na wewe unatarajia kuleta habari za kinyume. Kujadiliana kwanza inasaidia kuepukana na vita ya uhariri.

Nenda kwenye sanduku la mchanga na ubonyeze kiungo cha "*hariri chanzo*". Hii itafungua dirisha la kuhariria lililo na maandishi ya ukurasa huu. Weka kitu cha

---

tofauti kwenye ukurasa, na kama ni hivyo maelezo ya kupata viungo hayataeleweka moja kwa moja.

kujifurahisha au "Salam ulimwengu!", halafu **Hifadhi kurasa** na tazama nini ulichokifanya! Kuwa mwangalifu kuhakikisha kwamba unahariri ukurasa wa sanduku la mchanga, si maandishi ya ukurasa huu wa mwongozo.

# →Onyesha hakikisho→

Moja ya kipengele muhimu cha kuanza kutumia sasa ni kitufe cha **Onyesha hakikisho la mabadiliko**. Jaribu kufanya uhariri kwenye sanduku la mchanga, halafu bonyeza kitufe cha **Onyesha hakikisho la mabadiliko** badala ya **Hifadhi Kurasa**. Hii inakuruhusu kuona kurasa itakavyoonekana baada ya kuhifadhi, *kabla* hujahifadhi. Wote twafanya makosa; kipengele hiki kinakuonyesha makosa hayo. Kutumia Onyesha Hakikisho la Mabadiliko kabla ya kuhifadhi pia inakuruhusu kujaribu kubadili miundo na maharirio mengine bila ya kupagaranyua historia ya kurasa. Usisahau kuhifadhi maharirio yako baada ya kuhakiki!

# →Muhtasari wa kuhariri→

Kabla hujagonga **Hifadhi kurasa** ni adabu nzuri kuingiza maelezo mafupi sana kuhusu kile ulichobadilisha kwenye sanduku la **Muhtasari** lililopo baina ya dirisha la kuhariria na kitufe cha **Hifadhi kurasa**. Inaweza kuwa kifupi sana; kwa mfano kama unaingiza neno "typo", watu watajua kama umefanya masahihisho ya tahajia. Pia, iwapo mabadiliko uliyoyafanya kwenye kurasa yalikuwa

madogo, kama vile kusahihisha tahajia na makosa ya kisarufi, kuwa makini kutazama kisanduku cha "Haya ni mabadiliko madogo" (hii inapatikana ukiwa umeingia kwenye akaunti yako tu, basi).

## →Kufuatilia kazi yako→

Labda unapenda kuangalia makala ulipochangia kwa njia ya kuhariri au makala uliyoanzisha inaendelea jinsi gani kwa njia ya michango ya wengine. Hapa unaweza kubofya juu ya makala inaposema "**Fuatilia**". Ukiwa mwanawikipedia aliyejiandikisha makala hii imeingizwa sasa katika orodha yako ya maangalizi. Orodha hii naweza kutazama ukibofya "**maangalizi yangu**" na kibonye hiki kiko juu kabisa kwenye kila ukurasa wa wikipedia.

# Kuanzisha Makala

Ikiwa makala fulani hakuna, basi unaweza kuianzisha.

Kabla ya kuianzisha makala, hebu **ujiulize maswali yafuatayo**:

**A.**

1. Je ni afadhali kuanzisha makala mpya badala ya kuongeza makala iliyopo tayari?
2. Je una uhakika ya kwamba makala hii haiko bado? Labda kwa jina tofauti kidogo ? (Mfano: Westlands haiko, lakini kuna Westlands (Nairobi)). Lazima uchungulia kwa kutafuta jina kwa njia ya dirisha la kutafuta sehemu ya pili (ukitaipu "A" utaona kwanza orodha ya makala yanaoanza kwa "A" kama Afrika, Afrika Kusini, Asia - na chini yake "ya maneno...". Hapo chini unapata makala yote yenye neno unalotumia.
3. Je ni kweli makala inayofaa kwa wikipedia? Angalia Wikipedia:Umaarufu. (Mifano: makala juu ya shangazi yako haina mahali hapa kama shangazi huyu hajulikani nje ya ukoo na kijiji chake; makala inayoeleza neno fulani si kazi ya wikipedi lakini wikikamusi...)
4.

**B.**

Unatakiwa kuandaa makala yako ili kuwa na habari za maana na viungo vya lazima.

- Panga maandishi yako. Utangulizi inayojumisha habari za kimsingi katika sentensi 1-3, baadaye habari za undani zaidi.
- Tafuta kurasa za marejeo katika intaneti (=kurasa zenye habari za maana zitakazotajwa chini ya makala)
- Kumbuka pia makala yanayoweza kuhusiana na makala yako; uliweza kuziona (kama zipo) kwa kutumia dirisha la kutafuta jinsi ilivyoelezwa hapo juu na. 2. Ni vema kuweka viungo kadhaa kwa makala za maana. **Mfano:** Unaandika juu ya mtaa wa Daressalaam. Hapa ni lazima kuwega viungo kwa jina la mji, labda mitaa mingine muhimu iliyotajwa tayari, jina la wilaya yake, labda majengo au taasisi muhimu zilizopo hapa. Haitoshi kutaja majina haya, lazima kuweka viungo kwa umbo sahihi.
- Tafuta pia kama makala ya Kiingereza iko juu ya kichwa chako. Mara nyingi iko, na hapo utaifungua na kukopi orodha ya interwiki na kuibandika chini ya makala mpya.
- Soma orodha ya makosa ya kawaida na uepukane nayo.

**C.**

1. Kwanza kabisa **ujiandikishe** yaani uhakikishe ya kwamba una akaunti ya jina lako na umeingia kwa jina lako.
2. Afadhali **uandae makala katika nafasi yako ya mtumiaji**. Unda humo ukurasa mpya. Hapo fungua ukurasa wako wa mtumiaji, kwa kubofya jina lako linaloonekana juu kabisa kwenye dirisha la Wikipedia. Sasa unaona juu yake mstari wa URL (anwani ya intaneti) kwa mfano hivi: "*https://sw.wikipedia.org/wiki/Mtumiaji:Kipala*". Sasa ongeza humo nyuma ya jina lako "**/1**" itakayokuwa katika mfano "*https://sw.wikipedia.org/wiki/Mtumiaji:Kipala/1*". Bofya ENTER, utaona skrini mpya ambako unaweza kuchagua "Weka Chanzo" kwa kuunda makala yako ya jaribio. Katika nafasi hii uko huru kujaribu jinsi unavyopenda. Ukiridhika, bofya tena "Hariri chanzo" na peleka yote kwenye ukurasa wa makala mpya. Ona: Msaada:Jaribio
3. Andika jina la makala katika uwazi upande wa kulia. Thebitisha kwa kubofya "Anzisha makala yenye jina hili".
4. Sasa andika sentensi ya kwanza kwa namna ya kamusi: jina la makala kwa kawaida liwe neno la kwanza / maneno ya kwanza na kuonekana kwa herufi koza.

5. Mlango unaofuata katika mwongozo huu unakuelezea namna gani kupanga umbo la makala.
6. Chini ya makala weka sehemu ya "**Vyanzo**" au "**Marejeo**" kwa kutumia alama hizo: **==Marejeo== {{marejeo}}**
7. sasa panga makala katika jamii inayofaa (yaani kundi la makala zinazojumuiwa na kichwa).
8. Bofya "Onyesha hakikisho la mabadiliko" na sasa unaona umbo la makala jinsi itakavyoonekana.
9. Fanya masahihisho ya lazima halafu bofya "Hifadhi ukurasa".
10. **Interwiki**: Unganisha makala iliyohifadhiwa na **lugha nyingine za wikipedia**. Afadhali tafuta kwanza kama mada yako inapatikana katika wikipedia kwa lugha nyingine, kama Kiingereza. Kama hakuna, basi acha hatua hii. Kama unajua jina la Kiingereza, endelea hivyo: Chini kushoto unaona alama ya "Lugha" (picha chini), bofya "Ongeza viungo". Katika dirisha "Language" andika "enwiki", katika dirisha "Page" ndika jina la Kiingereza, thibitisha. (unaweza kuunganisha na lugha nyingine kama Kiingereza hamna)
11. Sasa fungua tena dirisha la hariri na kuingiza viungo kwa makala zilizopo tayari zinazohusiana na makala mpya (taz. juu).
12. Anzisha kila mstari mpya kwenye nafasi ya kwanza. Usiache nafasi tupu mwanzoni mwa

mstari mpya. Hii italetata matatizo itaonekana hivyo itasomeka vibaya:

**ANGALIZO:** Anzisha kila mstari mpya kwenye nafasi ya kwanza. Usiache nafasi tupu mwanzoni mwa mstari mpya. Hii italetata matatizo itaonekana hivyo itasomeka vibaya. Hatuitaki hapa.

*Menyu ya kuhariri jinsi inavyoonekana wavutini. Tazama picha chini.*




**D.**

Makala iliyoanzishwa nawe iko katika orodha ya "Maangalizi yangu" (unaona kiungo chake juu ya kila dirisha la wikipedia kama umeingia; kama huioni hujaingia bado!). Uiangalie wakati mwingine na tazama kama wasomaji wengine waliandika maoni au ushauri

kwenye ukurasa wa majadiliano. Hapa utaona pia kama kuna mtumaji amepinga maandisho yake, labda baada ya kuona kasoro nzito. Usisite kuwasiliana juu ya maoni haya.

**Jaribu kuhariri katika nafasi ya jaribio** ambayo inapatikana juu kabisa ya kila ukurasa. Jina ni ***"ukurasa wa majaribio."***

# Muundo

Kupanga umbo la maandishi ni tofauti kidogo na kuandika kwenye kichakata matini (programu ya kuandika) kama vile Word, Writer na kadhalika.

# Dirisha la hariri na WYSIWYG

Unaandika katika dirisha la uhariri. Humo huoni umbo la maandishi jinsi inavyotokea baadaye. Maana hapa hakuna kile kinachoitwa "WYSIWYG" ("What You See Is What You Get *unachoona ni sawa kile kinachotokea*").

Badala yake Wikipedia hutumia misimbo (codes) inayosababisha kutokea kwa maandishi manene, makubwa, madogo, ya rangi, vichwa au viungo na kadhalika. Hii ni lugha ya kompyuta ya pekee inayoitwa wikitext ikifanana na HTML lakini imerahisishwa.

# Herufi koze na *italiki*

Misimbo inayotumika hasa kwenye Wikipedia ni **Herufi koza**' ***na* italiki. *Yote mawili hupatikana kwa kuingiza neno / maneno kwa alama za apostrofi (*"**).

| Unaandika | Unapata |
|---|---|
| ''italiki'' | *italiki* |
| '''koze''' | **koze** |

| | |
|---|---|
| """koze italiki""" | ***koze italiki*** |

Kwa kawaida si lazima kutaipu apostrofi moja-moja. Unaweza kuangaza neno au maneno husika kwa puku yako na kutumia menyu (nembo dogo) juu ya dirisha la uhariri. "**B**" inakupa herufi koza, "*I*" inaleta herufi italiki.

Jina la makala ya Wikipedia inatakiwa kuonekana kwa herufi koza pale inapoonekana mara ya kwanza ndani ya makala, mara nyingi kama neno / maneno ya kwanza. Vinginevyo hatutumii herufi koza, isipokuwa ikisaidia kupanga matini marefu yasomeke vizuri zaidi pale ambako hatutaki kutumia vichwa vya habari.

**Mfano:** Makala ya Julius Nyerere inaanza:

"**Mwalimu Julius Kambarage Nyerere** alikuwa rais wa kwanza wa Tanzania. Alizaliwa Butiama, mkoani Mara pembezoni mwa Ziwa Nyanza tarehe 13 Aprili, 1922..."

*Herufi italiki* hutumiwa kwa ajili ya majina ya vitabu, filamu au albamu za muziki. Pia kwa kuonyesha matamshi ya neno la kigeni.

# Vichwa na vichwa vidogo

Vichwa na vichwa vidogo vya ndani ni njia ya haraka kuboresha mpangilio wa makala. Kama maandishi ni marefu kiasi ni afadhali kuingiza vichwa hivi. Ni muhimu kuwa na muundo 1 kwa makala zote maana hii inawasaidia wasomaji wasipate kuzoea uso mbalimbali ndani ya makala zetu.

> **Tahadhari 1:** Usiweke kichwa juu ya makala yako (yaani mwanzoni wa maandishi yote) kwa sababu wikipedia inafanya hii pia!

> **Tahadhari 2:** Usiweke vichwa nje ya utaratibu huu: usitumie mstari yenye **HERUFI KUBWA** au **mstari mwenye maandishi koza** kama vichwa vya ndani.

Vichwa huanzishwa kwa njia hiyo (hakuna alama kwa kazi hii kwenye menyu)

| Unaandika | Unapata |
|---|---|
| == Kichwa == | **Kichwa** (kichwa kikubwa) |
| === Kichwa kidogo 1 === | **Kichwa kidogo 1** |
| ==== Kichwa kidogo 2 ==== | **Kichwa kidogo 2** |

Kama vichwa 4 au zaidi vimeshaingizwa katika makala sanduku ya yaliyomo inaanzishwa na programu peke yake. Tazama juu: sanduku hili limejitokeza tu bila kazi ya ziada kwa sababu kuna vichwa vinne kwenye ukurasa!

# Makosa ya kawaida

Makosa hutokea na wewe hutakuwa mtu wa kwanza kwenye wikipedia kufanya makosa. Lakini sisi sote tunapenda kuboresha wikipedia na uwezo wetu wa kuchangia. Ili ujifunze juu ya makosa yanayotokea mara kwa mara angalia Wikipedia:Makosa!

Jaribu kuandika kichwa kwenye sanduku la mchanga wa ukurasa huu.

**Jaribu ulichojifunza katika aukurasa wa majaribio.**

# Viungo vya Wikipedia

**Kuunga** pamoja viungo vya makala za Wikipedia ni kazi nyepesi lakini muhimu sana. Inaruhusu watumiaji kupata habari nyingi zinazohusiana na makala wanayosoma. Inaongeza manufaa ya Wikipedia kwa wasomaji.

**Mfano**

**Viungo vya buluu**

Makala juu ya mji wa Misri inaweza kuonekana hivyo:

> **Giza** (Kar.: الجيزة *al-gīza*) ni mji wa kaskazini mwa Misri unaopakana na mji mkuu Kairo. Inajulikana hasa kama mahali pa piramidi.

Maneno yenye rangi ya buluu yanaunga makala hii na makala nyingine kuhusu Kar. = Kiarabu, Misri, Kairo na piramidi. Ukibofya neno la buluu unapelekwa kwenye makala hizo.

**Viungo vyekundu**

Kuna pia viungo vyenye rangi nyekundu:

> **Mabata-bahari** ni ndege wa maji wa familia ndogo ya Merginae katika familia ya Anatidae.

Katika sentensi hii makala za ndege, Merginae na Anatidae ziko tayari lakini "familia ndogo" haikuandikwa bado.

Wakati wa kuandika makala unaweza kuanzisha viungo vyekundu ukiona hapa ni neno muhimu inayostahili makala yake.

Hapa unatakiwa kuwa mwangalifu


- usiweke maneno hovyo katika mabano mraba na kuanzisha kiungo chekundu maana maneno yaleyale katika mabano yanatakiwa kuwa jina la makala mpya.
- fanya utafiti kama mada iko tayari labda kwa tahajia tofauti; kwa mfano umetafuta nchi ya "Aljiria", kumbe: "Algeria" iko tayari!

**Jinsi ya kuunga**

**Mabano mraba [[ ]]**

Ili kuunganisha ukurasa mmoja na mwingine wa Wikipedia (inaitwa *kiungo cha wiki*), weka katika mabano mraba mawili, kama hivi:

Mfano: [[Televisheni]] = Televisheni.

Njia nyingine kwa kutumia puku ni kuangaza maneno husika na kubofya alama ya  kwenye menyu ya dirisha la uhariri.

**Kigawanyishi-kibomba "|" kwa umbo tofauti la neno**

Mara kwa mara jina la makala inayoelekezwa ni tofauti kidogo na maneno katika makala unayoshughulikia kama tofauti umoja/uwingi.

Mfano: "Serengeti kuna **viboko** wengi...". Unataka kuweka kiungo kwenda makala ya mnyama "**kiboko**".

Hapa unaweza kugawa mabano mraba kwa kutumia alama ya kigawanyishi-kibomba "|" (SHIFT + BACKSLASH kwenye baobonye zenye ABC za Kiingereza). Sasa kuna sehemu mbili ndani ya mabano mraba. Nafasi ya kwanza unaandika jina la makala inayoelekezwa na nafasi ya pili nyuma ya kigawanyishi unaandika maneno jinsi yanavyofaa katika sentensi yako.

Mfano: **[[Kurasa uliyoilenga|maandishi yanayoonekana]]** = maandishi yanayoonekana

Pia unaweza kutengeneza kiungo kuelekea sehemu mahususi ya makala kama kuna vichwa vya ndani ya makala:

[[Makala unapolenga#Sehemu ya makala yenye kichwa kidogo|maandishi yanayoonekana]] = maandishi yanayoonekana

**Kiungo kuonekana kama *italiki* au koze**

Iwapo unataka "maandishi yanayoonekana" ya kiungo kuonekana kama "italiki" (yaani herufi mlazo), weka apostrofi mbili kabla na baada ya mabano mraba kama hivi:

''[[Mapinduzi ya Viwandani]]'' = *Mapinduzi ya Viwandani*

(ukizoea utaangaza sehemu ya mabano mraba na kubofya alama ya " *I* " kwenye menyu ya kuhariri. Vilevile kwa kiungo kuonekana kama koze).

**Kuhakikisha viungo ni sahihi**

Hapa tunatumia dirisha la "tafuta" 

upande wa kushoto. Tukitaka kujua kama kuna chochote tayari kuhusu "Pemba" tunaandika neno hili dirishani. Halafu tunabofya "tafuta" tutapata orodha ya makala 119 yote yaliyo na neno "Pemba" ama katika jina au katika maandishi ya makala, kama vile Pemba (kisiwa), Mkoa wa Pemba Kusini, Mkoa wa Pemba Kaskazini, kata zote za Pemba, makala za kihistoria zinazogusa Pemba na mengine. Kwa kuchungulia usigonge "makala" chini ya dirisha maana hii itakupa makala 1 tu ama ya Pemba (maana) au ya mahali 1 tu. Kwa njia hii unaweza kuunganisha na makala yaliyopo tayari ukitumia jina na umbo sahihi.

Tafadhali tazama viungo vyako ili kuhakikisha kwamba zimeelekezwa katika makala sahihi. Kwa mfano, Gibraltar imelengwa katika makala inayohusu eneo dogo la Kiingereza ndani ya Hispania, wakati Mlango wa Gibraltar ni jina la makala inayohusu mlango wa bahari kati ya Ulaya na Afrika karibu na Gibraltar.

Pia kuna kurasa za kutofautisha "maana" -- hizi siyo makala, bali kurasa zenye viungo vya makala zenye majina ya karibu. Tazama Msaada:Maana kwa kuanzisha makala hizi.

**Makosa ya mara kwa mara**

Makosa yanatokea kwa urahisi usipoangalia vema yote ndani ya mabano mraba. Usiweke mabano ya kiungo bila kutafakari. Usimwage matokeo ya google translate bila kuchungulia kwanza!

Kwa mfano kuingiza alama za **.** au **,** ndani ya kiungo inabadilisha marejeo na kuharibu kiungo. [[Afrika,]] haiwezi kuunganisha na Afrika kwa sababu ya koma ndani ya mabano.

Lingine ni kutumia umbo la neno lisilo kawaida kwa mfano wingi badala ya umoja au kinyume. Hapa ni sharti kuchungulia kupitia dirisha la tafuta au jamii: je, umbo la kawaida hapa ni nini? Vilevile tahajia isiyo kawaida.

Jaribu kutafuta majina ya kikamusi; usiweke kiungo kwa "biashara haribifu ya watumwa". Jina la kikamusi ni "biashara ya watumwa".

### Viungo vya picha

Picha au michoro huonekana katika makala kwa njia ya viungo. Kwa maelezo zaidi soma **Msaada:Picha**

### Wakati wa kuunga

Kuongeza viungo kwenye makala kunaleta maana zaidi, lakini viungo vingi mno huleta vurugu. Utaratibu ni huu: fanya neno fulani mara moja tu kuwa kiungo katika makala moja, usirudie neno hili kama kiungo. Unapaswa kuchagua mara ya kwanza ambako neno hilo linatokea kwenye makala.

Kuchungulia kwenye viungo vingine vya makala za Wikipedia pia inaweza kukusaidia kujifunza wakati wa kuweka viungo. Tazama ukurasa wa makala nzuri kwa orodha ya makala zenye ubora mkubwa.

### Jamii au Category


Kila makala inatakiwa kuungwa katika jamii na makala nyingine zinazojadili mada za karibu.

> Andika [[Jamii:]], na weka jina la jamii nyuma ya "nukta pacha" baina ya mabano ya miraba miwili.

**Ni muhimu sana kuweka jamii sahihi, kwa kuwa hivyo itakuwa rahisi kwa watu wengine kupata kazi yako.** Njia iliyo bora ya kutafuta jamii gani inayotakiwa iwekwe kwenye makala ni kuchungulia kurasa zenye kuelezea suala moja, na tazama jamii gani walizotumia.

> Mfano: Unaandika makala kuhusu mnyama fulani. Chungulia kwa kuandika "**jamii:wanyama**" katika dirisha la "tafuta" na angalia vijamii vidogo vilivyopo tayari na makala zilizo ndani ya vijamii hivi.

# Interwiki




Bofya hapa kuona picha vizuri zaidi

Interwiki ni orodha ya viungo vya mada fulani na makala za kufanana katika Wikipedia za lugha mbalimbali. Katika ukurasa unaosoma sasa hivi orodha ipo upande wa kushoto nje ya makala chini ya kichwa "Lugha nyingine". Hapo unaona majina kama Alemannisch, العربية, Català, Česky, English na kadhalika. Zote ni za rangi ya buluu maana ni viungo vya kwenda kurasa za "Mwongozo wa Wikipedia" kwa lugha hizo.

Ukianzisha makala mpya na kuihifadhi utaona hakuna majina ya lugha ya buluu bado. Ukibofya pembeni "Add links" utaona dirisha dogo. Humo unaandika juu "enwiki" na kuthibitisha, chini yake unaandika jina la makala husika katika Wikipedia ya Kiingereza. Thibitisha tena

mara mbili na sasa makala yako ya Kiswahili imeunganishwa na namba ya mada yake katika orodha "Wikidata" inayoorodhesha makala za Wikipedia zote. Sasa itaonyesha lugha nyingine kwa rangi ya buluu na makala yetu ya Kiswahili inaonekana pia kwa wasomaji wa lugha hizo nyingine. Huu ni msaada mkubwa kwa wahariri wanaoweza kusoma lugha mbalimbali na kuongeza habari kutoka huko.

Ukikuta kiungo cha Interwiki kisicho sahihi (mtumiaji aliyetangulia alikosa kuteua namba sahihi) unaweza kubofya "Hariri viungo". Sasa unafika katika ukurasa wa Wikidata, angalia sanduku ya "Wikipedia", bofya "edit" halafu alama ya ndoo ya takataka ili kufuta neno la Kiswahili. Sasa bofya "publish" na kufunga Wikidata. Ukiita sasa makala yako utaona haionyeshi interwiki tena (inaweza kuchukua dakika kadhaa hadi mabadiliko yanaonekana). Sasa unaweza kuanza upya kuweka interwiki sahihi.

Hatua hizo utatekeleza katika mtazamo wa dawati (Desktop view) inayopatikana kwa kubofya maandishi madogo "dawati" kwenye dirisha la simu yako, chini kabisa.

# Kutaja Vyanzo

Vyanzo vya habari ni mahali tunapopata habari zetu za hakika. Katika Wikipedia vyanzo hivyo vinatakiwa kuonekana maana habari zisizo na vyanzo kuna uwezekano mkubwa wa kuondolewa.

Katika Wikipedia yetu mara nyingi si rahisi kuonyesha vyanzo kwa sababu wachangiaji wengi hawana nafasi ya kutumia maktaba nzuri zenye majarida na vitabu vya kitaalamu.

Kwa hiyo tunatumia mara nyingi vyanzo visivyo vya Kiswahili, na hasa vya Kiingereza. Ni sawa kunakili orodha ya vyanzo kutoka makala ya en:wikipedia. Kuna pia vyanzo vizuri vinavyopatikana mtandaoni.

**Kumbuka: makala ya wikipedia si vyanzo vinavyokubalika! Lakini unaweza kutumia vyanzo vinavyotajwa katika makala za enwiki.**


**Tanbihi chini ya ukurasa**

Njia nyepesi ya kuonyesha chanzo cha habari ni tanbihi (*footnotes*) chini ya ukurasa. Hapa kuna alama



kwenye menyu ya kuhariri chanzo.

Ukibofya hapa unafungua dirisha la




.

Sasa andika chanzo au maelezo mengine katika nafasi yake chini ya maneno "Maandishi ya marejeo".

Bado hatua moja: chini ya makala mwishoni andika:

**===Marejeo===**

{{marejo}} AU <references/> **AU** {{reflist}}

Hapo vyanzo ulivyotaja kwenye mabano au maelezo juu vitaorodheshwa chini ya kichwa hicho.

Kama chanzo chako ni tovuti ya intaneti (nje ya Wikipedia) fanya hivyo:

- weka **kiungo cha nje** kwa kuandika mabano mraba **[ ]** - mara moja tu, si mara mbili jinsi ilivyo kwa viungo vya makala nyingine za Wikipedia! Kati ya mabano hayo uingize anwani ya intaneti au URL (unaweza kutaipu pia), kwa mfano [http://www.example.com] (jina la kiungo)
- andika anwani ya tovuti kati ya mabano mraba, acha nafasi tupu 1,2 kabla ya mabano ya pili halafu ongeza maneno ya maelezo

[http://www.example.com **Maelezo yanayoonekana**]

Usitaje makala nyingine ya Wikipedia kama chanzo lakini unaweza kunakili vyanzo kutoka huko KAMA VINAFAA. Kwa mengine ona: Msaada: Marejeo na kutaja vyanzo

**Marejeo tata kutoka Wikipedia ya Kiingereza**

Mara nyingi tukitafsiri makala ya Kiingereza tunakuta marejeo tata ambayo hayawezi kunakiliwa katika swwiki.

Kwa mfano marejeo yanayoonyesha kitu kama **<refname= JINAFULANI> texttext<ref>** au {{**cite rowlett|mdg**}} ambacho hakiwezi kunakiliwa katika Wikipedia yetu.

Fanya hivi: Fungua makala ya swwiki na pia ya enwiki iwe kando yake. Kwenye makala ya enwiki fanya rightclick kwenye sehemu ya buluu ya tanbihi (footnotes/reference), ili upate tab ya tovuti inayorejelewa.

Ukiwa kwenye dirisha la "Hariri chanzo" (source edit), kopi URL (anwani ya intaneti) na kuiweka kati ya mabano makali **<ref>[xxxxxxx yyyy]</ref>**. xxxx ni URL unaokopi, yyyy ni matini ya tanbihi kutoka enwiki. Acha nafasi tupu baina xxx na yyy.

Ukitumia "Chanzo" (visual edit) bofya "Cite" halafu Manual na kuchagua Basic. Pale unaweka URL (xxxx) na baada ya kuacha nafasi, unaingiza matini unayotaka kuonyesha katika tanbihi (yyyy).

**Viungo vya nje**

Makala nyingi za Wikipedia huwa na sehemu mwishoni inayoitwa "Viungo vya nje".

Hapa tunaweka viungo vya nje kwa tovuti zenye maana na zinazokubalika zinazohusu kichwa na yaliyomo ya makala..

Inatosha kutaipi anwani kamili ya tovuti unayotaka kurejea:

http://www.britannica.com/EBchecked/topic/336408/Leonardo-da-Vinci

# Namna ya kutaja vyanzo

- Kutaja **marejeo katika kitabu**: Utataja jina la mwandishi, jina la kitabu, mwaka wa kuchapishwa na mahali pake, kampuni ya kuchapisha, ukurasa au kurasa penye habari unazorejelea
- Kutaja **marejeo katika gazeti au jarida**: utataja jina la mwandishi (kama lipo), kichwa cha makala, jina la gazeti/Jarida, tarehe yake
- Kutaja **marejeo kutoka intaneti**: utataja jina la mwandishi (kama lipo), kichwa cha makala, jina la tovuti, tarehe yake, unaongeza tarehe ulipoangalia tovuti, URL (=anwani ya intaneti). Huwezi kutumia tovuti yoyote. Facebook, twitter na "social media" kwa jumla si vyanzo vinavyofaa kuunda umaarufu au umuhimu wa habari.

# Kurasa za Majadiliano

Kila makala ya wikipedia huwa na "Ukurasa wa Majadiliano". Hii ni sehemu muhimu ya mradi huu na msaada mkubwa wa kuelewana kati ya wanawikipedia na kwa kuboresha makala.

**Ukurasa wa majadiliano wa makala**

Hapa ni mahali pa kuweka maswali, mapendekezo au maoni juu ya makala - si ndani ya makala!!

**Ukurasa wa majadiliano wa watumiaji**

Sio kila makala tu hata kila mtumiaji huwa na ukurasa wa majadiliano. Hapa unaweza kuacha ujumbe kwa mtumiaji mwingine.

Kama mtu ameache ujumbe kwenye ukurasa wako utaona sanduku lenye maneno ya kutangaza ujumbe mpya kwako kila ukiingia wikipedia kwa jina lako.

Kuna njia mbili za kujibu ama kwenye ukurasa wako ulipopata swali la mtu mwingine au kwenye ukurasa wake. Ukijibu kwake ataiona akijisajili tena.

**Kupanga maandishi yako kwenye kurasa za majadiliano**

Unaingia kwa kubofya alama ya "majadiliano" juu ya ukurasa wa uhariri. Usijali kama rangi yake ni nyekundu

maana hakuna aliyefungua ukurasa huu na wewe utakuwa mchangiaji wa kwanza.

Ukikuta maandishi tayari weka maandishi yako chini yale yaliyotangulia. Kama unaanzisha mada mapya ni vema kuingiza mstari wa kichwa cha ndani kwa mfano

> ==Msaada wa makala baobonye==
>
> Salaam nimeona wewe ni mtaalamu wa kompyuta naomba usaidie makala ya baobonye.

Unatakiwa kutia sahihi chini ya jibu lako ama kwa kuandika ~~~~ au kubofya alama  katika menyu ya ukurasa wa uhariri.

Si lazima lakini unashauriwa kujiandikisha kwanza kwa jina fulani. Hii haileti gharama kwako lakini utajulikana zaidi inasaidi mawasiliano.

**Kujongeza ndani**

Ukiingia katika majadiliano na majibu ni vema kutofautisha michango kwa kujongeza ndani. Kawaida ni kujongeza kila jibu hatua moja. Hii inaendelea hatua moja-moja hadi nafasi ya jibu imekuwa nyembamba mno halafu kurudi mbele tena.

Unajongeza maandishi yako ndani kwa kuandika alama ya nukta pacha (:) kwenye nafasi ya kwanza ya mstari na kuandika baadaye. Nukta pacha 2,3,4 zinasukuma maandishi ndani zaidi. Ukianzisha mstari mpya au kuweka alama ya inamaliza kujongeza ndani. Ukitaka kutumia ibara ndani ya mchango wako unahitaji kurudia

nukta pacha mwanzoni wa ibara mpya sawa na ibara ya kwanza.

Mfano:

Mstari huu haukujongezwa ndani.

: Nukta pacha inasababisha kujongezwa ndani

:: Mstari huu umejongezwa ndani hatua 2 kwa kutumia nukta pacha 2

itaonekana vile: Mstari huu haukujongezwa ndani.

Nukta pacha inasababisha kujongezwa ndani.

Mstari huu umejongezwa ndani hatua 2 kwa kutumia nukta pacha 2

**Alama nene kwa orodha**

Ukiandika orodha unaweza kutofautisha mistari kwa alama nene kwa kutumia alama ya kinyota (*) mwanzoni. Kuweka kinyota mara mbili inajongeza mstari ndani pia.

Mfano:

* Mstari wa kwanza

* Mstari wa pili

** Kifungo cha chini cha mstari wa pili

* Mstari wa tatu

itaonekana hivyo:

- Mstari wa kwanza
- Mstari wa pili
    - kifungo cha chini ya mstari wa pili

- Mstari wa tatu

**Orodha yenye namba**

Orodha yenye namba mfululizo unapata kwa kutumia alama hii: (#). Hata hapa unaweza kutumia alama mbili kwa kuonyesha mistari za ndani.

Mfano:

# Jambo la kwanza

# Jambo la pili

## Nyongeza chini ya jambo la pili

# Jambo la tatu

itaonekana vile:

1. Jambo la kwanza
2. Jambo la pili
    1. Nyongeza chini ya jambo la pili
3. Jambo la tatu.

# Kumbuka

**Taratibu na kawaida kwenye wikipedia**

Kuna machache ambayo unatakiwa kukumbuka ukichangia na kuhariri kwenye wikipedia.

**Umuhimu: Kuandika juu ya nini?**

Wikipedia ni kamusi elezo. Kwa hiyo tunalenga kukusanya habari zinazofaa kwa kamusi elezo. Maana yake makala yanatakiwa kuhusiana na mada yenye umuhimu fulani.

Wanawikipedia wanaendelea kujadiliana umuhimu ni nini. Kwa jumla tuko pamoja ya kwamba haifai kuwa na makala juu ya mtu yeyote anayeishi au aliyeishi duniani, au kuhusu kila barabara za miji yote au kuhusu kila kampuni inayouza kitu kwenye sayari hii. Kwa hiyo tutaendelea kujadiliana "umuhimu" ni nini ila tu ujiandae kutetea chaguo lako na usikate tamaa kama makala juu ya shangazi yako inafutwa na wengine !

Kamusi elezo si sawa na kamusi ya lugha. Kwa hiyo makala zinazoeleza maana ya neno tu si shabaha yetu. Kuna mradi ndugu wa Wikamusi kwa kamusi ya lugha ingawa ni changa bado.

Pia maandishi marefu kutoka kitabu -ama kitabu chako mwenyewe au kitabu kinachopatikana kama maandiko huria kwenye intaneti hayafai kuingizwa vile hapa wikipedia. Kuna mradi mwingine kwa maandishi ya aina

hii ambao unaitwa Wikisource. Lakini nukuu fupi inakubalika.

## Miradi ndugu ya wikipedia

Kuna miradi mingine iliyoanzishwa pamoja na wikipedia ingawa sehemu kubwa bado haiko kwa Kiswahili:

| | | |
|---|---|---|
| **Commons**<br>Ghala ya Nyaraka za Picha na Sauti | **Meta-Wiki**<br>Uratibu wa Miradi yote ya Wikimedia | **Wikamusi**<br>Kamusi na Tesauri |
| **Wikitabu**<br>Vitabu vya bure na Miongozo ya Kufundishia | **Wikidondoo**<br>Mkusanyiko wa Nukuu Huria | **Wikisource**<br>Nyaraka Huru na za Bure |
| **Wikispishi**<br>Kamusi ya Spishi | **Wikichuo**<br>Jumuia ya elimu | **Wikihabari**<br>Habari Huru na Bure |

Kwa orodha ya miradi yote tazama Complete list of Wikimedia projects kwa Meta.

## Yasiyofaa

### Wikipedia si mahali pa:

- **kuonyesha matokeo ya utafiti asilia** yaani habari ambazo wewe kama mwandishi umebuni

mara ya kwanza au **nadharia mpya** zisizoangaliwa bado na wataalamu wengine. Maana yake kama wewe umegundua ukweli fulani wikipedia si mahali pa kuitangaza mbele ya dunia. Tunapendelea kusubiri hadi wataalamu wengine wameiangalia na kuchangia mawazo yao.

- **kujitangaza**. Kama wewe ni mwandishi, mwimbaji au msanii bora haifai ukieleza ubora wako mwenyewe. Subiri tu kidogo hadi wengine wanakujua na kuimba sifa zako!
    - Usianzishe makala juu yako mwenyewe katika sehemu ya kamusi! Unaweza kutumia nafasi ya ukurasa wako wa mtumiaji. Hapa uko huru kuleta habari juu yako. Nje ya hapo ni marufuku! (soma zaidi hapo: Wikipedia:Ukurasa wangu na kurasa za kamusi)
    - Usitaje jina lako katika makala kama mwandishi.
- **kutangaza biashara, kuhubiri juu ya dini au siasa**
- **kutukana wengine.**

### Msimamo wa kutopendelea upande

Sheria muhimu katika wikipedia "**Msimamo wa kutopendelea upande**. Sheria hii inasema ya kwamba tunakubali kutaja maoni mbalimbali yenye maana juu ya mada fulani.

1. Si mahali pa kumsifu au kumpinga mtu au kitu chochote. Si mahala pa kusambaza maoni kama ukweli.
2. Ni sawa kutaja maoni lakini sharti maoni yaonekana vile tusiyaonyeshe kama ukweli halisi.
3. Tusiandike: "Bwana fulani ni mwanamichezo bora wa Afrika". Hii ni hoja, si bayana ya hakika. Kama ni kweli na muhimu, andika ya kwamba "Kuna watu wanaomwona kama mwanamichezo bora wa Afrika". Lakini kama huwezi kutaja ushuhuda au vyanzo *(taarifa ya gazeti inayopatikana katika intaneti au kitabu)* kuwa amesifiwa hivyo uwezekano ni mkubwa ya kwamba sentensi kama hii itafutwa.
4. Tujaribu kuchukua msimamo wa kati yaani tueleze mitazamo na maoni mbalimbali yaliyopo kama ni muhimu.

Msimamo huu ni muhimu hasa kwenye mada kama dini au siasa ambako maoni hutofautiana mara nyingi.

Kwa ushauri zaidi unaeza kuangalia majadilianoi kwenye wikipedia ya Kiingereza kama vile: Staying cool when the editing gets hot na pia Wikipedia:NPOV_tutorial.

### Kutaja vyanzo

Kumbuka ukurasa wa Wikipedia:Mwongozo (Kutaja vyanzo)!

### Haki za hatimiliki

- Usiingize picha au maandishi ambako mtu fulani ana hakimiliki bila kibali chake!
- Usinakili na kumwaga maandishi kutoka tovuti nyingine katika makala! Tumia maneno yako mwenyewe. Hata maandishi ya intaneti huwa na haki za hatimiliki.
- ukitafsiri makala ya wikipedia ya lugha nyingine au kuchukua picha kutoka huko ni halali.

**Uungwana wa wikipedia**

Wikipedia inaomba wachangiaji wote watendeane an kujadiliana kwa heshima. Hata kama mawazo yanatofautiana kumbuka hii!.

Wote hapa wanajitolea bila malipo. Ukimwona mtu akifanya jambo la ajabu au kosa umwandikie kwenye ukurasa wa majadiliano ya makala na kwenye ukurasa wa majadiliano wa mtumiaji.

Linganisha Wikipedia:Etiquette.

**Kubadilisha jina la makala ?**

Wakati mwingine utakuta makala unapofikiri ya kwamba jina lake si sahihi. Ama mwandishi alikosa tahajia au jina lenyewe au kwako mada hii inajulikana zaidi kwa jina tofauti.

1. Usinakili yaliyomo ya makala na kuiweka kwa makala mpya yenye jina nyingine!! Hii ni kosa kubwa. Hasa kwa sababu inafuta historia ya makala na viungo vilivyopo tayari.
2. Unaweza kuhamisha makala kwenda jina jipya baada ya kutafuta majadiliano na

wengine. Jaribu kupatana na wahariri wengine kwanza. Kwa hiyo unaandika hoja lako kwenye ukurasa wa majadiliano. Usisahau kutaja kifupi pendekezo lako kwenye mstari wa "muhtasari" (chini ya dirisha la kuhariri). Na angalia kwenye historia ya makala ni nani mhariri aliyetunga makala, unaweza kuchungulia kama yuko bado na kumwomba asome pendekezo lako.

Baadaye unaweza kuhamisha makala kwenda jina jipya kama umejiandikisha sawasawa. Heri usihamishe kurasa za "maana". (Linganisha en: How to rename (move) a page.

1. Wakati mwingine njia inayofaa ni kuanzisha ukurasa wa kuelekeza. Hapa unafungua ukurasa mpya kwa jina unalofikiri ni sawa au afadhali ndani yake unaweka tu kielekezo. Mfano: Unakuta ukurasa wa nchi "Cote d'Ivoire"; unafikiri afadhali iwe "Aivori Kost" maana umeona umbo hili la jina. Basi unanzisha makala ya "Aivori Kost", na ndani yake unaandika tu

#REDIRECT [[*Cote d'Ivoire*]]

(unaweza pia kubofya alama ya  na kuingiza jina la ukurasa husika uliopo tayari , katika mfano "Cote d'Ivoire". Kila anayetafuta "Aivori Kost" atafika "Cote d'Ivoire")

**Kuonya na kubana**

Kwa bahati mbaya tunakuta mara kwa mara wachangiaji wasiofuata ushauri na kuleta makala zisizolingana na kanuni zetu. Wakabidhi wa wikipedia hii wanajaribu kuwashauri, kama lazima pia kuwaonya. Wasipofuata maonyo, wanaweza kubanwa kwa muda fulani au milele. Wako pia watumiaji wanaoleta uharabu kwa kufuta maudhui au kuigiza upuuzi; wakionekana wamefanya haya kwa makusudi wanabanwa. Kila mwanawikipedia ana haki ya kupinga kama amebanwa. Kimsingi wakabidhi wanajaribu kufuata kanuni zinazoelezwa kwa Kiingereza hapa simple:Wikipedia:Blocks_and_bans (kwa kifupi katika simple.wikipedia) au hapa en:Wikipedia:Blocking_policy (kwa kirefu, enwiki). Orodha ya waliobanwa inaonekana hapa Maalum:Kumbukumbu/block.

# Kujisajili

**Kujisajili kama mtumiaji**

Kila mtu anaweza kuchangia kwenye Wikipedia hata bila kujiandikisha.

**1. Faida za kujisajili**

Kujisajili kunaleta nafasi za nyongeza na faida hasa ukichangia mara kwa mara. Hasa:

- unapata nafasi zaidi za kuhariri, kwa mfano kama ukurasa umehifadhiwa
- unapata ukurasa wa "Maangalizi yangu" unaosaidia kutazama makala unazopenda kufuatilia.
- unaweza kuhamisha kurasa (lakini kumbuka sheria zake)
- ni rahisi kutambuliwa na kuheshimiwa na wengine kwa sababu wanakujua kutokana na michango yako
- wengine wanaweza kuwasiliana nawe kwenye ukurasa wako wa majaidiliano

**2. Kufungua akaunti**

- Hatua ya kwanza ni kubofya kwenye kona ya juu 

na baadaye tena kwa "kujisajili".

- Kwa usalama wa Wikipedia ni lazima kutaipu herufi zinazoonyeshwa katika dirisha dogo chini yake.
- Sasa unaingiza jina ulivyojichagulia na nywila (neno lako la siri) mara mbili.
- **anwani ya baruapepe** si lazima; lakini unashauriwa kuiandikisha! Inasaidia kama unapenda kuwasiliana na watumiaji wengine kwa njia hiyo. Unaweza pia kuiacha kwanza na kuiongeza baadaye.
- Mwishoni unabofya chini "sajili akaunti"
- Kama jina ulilochagua limeshachukuliwa na mwingine au kama umekosea kutaipu neno la siri mara mbili unaona dirisha unapaswa kuanza upya.

**3. Kuingia**

- Ukiwa mwenye akaunti na jina la Wikipedia unaweza kuingia kila safari unapofungua Wikipedia.
- Unabofya tena kwenye kona ya juu utapata dirisha la "Ingia".
- Sasa unaona viungo vipya kwenye mstari wa juu kabisa kama vile
    - Jina lako - inafungua ukurasa wako binafsi
    - Majadiliano yangu - inafungua majadiliano kwenye ukurasa wako
    - Mapendekezo yangu - hapa unaweza kubadilisha kuonekana kwa kurasa zako

    - Maangalizi yangu - inaonyesha orodha ya makala uliyochagua kufuatilia mabadiliko yao
    - Michango yangu - inakupa orodha ya michango yote uliyofanya kwenye Wikipedia
    - Toka - ukipenda kutoka kwa safari hii - baada ya kubofya hutakuwepo tena kwa jina hadi kuingia tena
- Kama mwandishi aliyejiandikisha utaonekana kwa watumiaji wote wengine - kwa mfano hivyo: Bofya hapa na andika jina la mtumiaji

**4. Kuwezesha baruapepe**

- Hakikisha kwamba umeingiza anwani yako ya baruapepe
- Bofya menyu "Mapendekezo" *("preferences")*
- Tafuta chini "Hitiari za barua pepe"
- Bofya "Yakinisha anwani yako ya barua pepe"
- Sasa fungua baruapepe zako, utaona ujumbe kutoka Wikipedia / Wikimedia.org
- Thibitisha kwa kubofya "Confirm email address"
- Sasa kila mtumiaji aliyejiandikisha ataona menyu "Email this user" kwenye ukurasa wako. Anaweza kukuandikia lakini haoni anwani yako.

**TAMATI**